

# HALMASHAURI YA MJI HANDENI



## SHULE YA SEKONDARI KIVESA

**KUMB.NA.HDC/S.1930/J.10/**

**KWA MZAZI/MLEZI**

**MAAGIZO YA KUJIUNGA KIDATO CHA KWANZA MWAKA 2021**

**1.0** Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao.....amechaguliwa kuingia kidato cha kwanza shule hii mwaka 2021.Hongera sana kwa Mwanao kupata nafasi hii muhimu kwa maandalizi ya maisha yake ya badae.Ni matumaini ya Shule kuwa mwanao ataitumia nafasi hii vizuri.

**2.0:Shule itafunguliwa kwa muhula wa kwanza Tarehe 11/01/2021.**Mwanao anatakiwa kuripoti shuleni siku hiyo saa **01:00 asubuhi** bila kukosa akiwa na mzazi/mlezi wake.

**3.0:**Shule hii ni ya kutwa (**Day school**) hivyo mwanao atalala Nyumbani na kuja Shuleni kila siku Asubuhi na kurudi nyumbani baada ya shughuli za shule za siku kuisha.Kama utampangishia chumba mwanao hakikisha unaweka uangalizi wa karibu kwa mwanao vinginevyo utapata hasara.Usifanye kosa la kumwamini mwanao sana kwani Handeni ina mazingira ya kimjini na vishawishi ni vingi.

### **4.0 SARE ZA SHULE**

**4.1**Mwanafunzi awe na shati mbili(2) nyeupe za mikono mifupi

### **WAVULANA**

Suruali mbili(2) kwa wavulana na sketi mbili(2) kwa wasichana.Zote ziwe na rangi ya kijani iliyokolea kitambaa kimeambatanishwa.

**MSHONO:**Suruali ishonwe kawaida ikiwa na mifuko mitatu(3),Marinda mawili(2) kulia na kushoto na luksi sita(O6) tu.Mkanda wa kuvalia suruali uwe mweusi

***NB:Suruali pana isiyobana yenye mapana yasiyopungua inchi kumi na saba(17) na yenye turn-up***

### **WASICHANA**

**Sketi mbili za rangi ya kijani iliyokolea(dark green)**

### **MSHONO.**

.Kwa wasichana sketi iwe ndefu yenye rinda boksi (ukubwa wa rinda boksi usizidi inchi mbili au tatu).Vazi la hijabu na nusu kanzu vizingatie sare ya shule(***kitambaa cheupe cha tetroni***)

**ANGALIZO:**Zingatia rangi na maelekezo ya mshono.Mishono na staili zingine hazitakubalika

**4.2:**Viatu vya kawaida vya ngozi **vyeusi** kwa Wavulana pamoja na soksi nyeusi,soksi nyeupe kwa wasichana.Viatu visiwe na visigino virefu.Vilevile awe na raba za michezo

**4.3:**Mwanafunzi awe na fulana ya shule rangi **kijivu** yenye nembo kwa ajili ya shughuli za nje ya darasa kama michezo na kazi za mikono

#### **4.4:SWETA:**

Mwanafunzi awe na sweta la rangi ya **kijani iliyokolea(dark green)** kwa ajili ya kujikinga na baridi rangi nyingine haziruhusiwi.

#### **5.0:MAHITAJI MENGINE**

**5.1:**Mahitaji ya darasani:Mwanafunzi awe na daftari 20 za notsi na mazoezi,kalamu,futio,rula na mkebe wa mahesabu(mathematical set).Kila mwanafunzi awe na mfuko wa shule(schoolbag) kwa ajili ya kuhifadhi na kubebea vifaa vya shule.Ni marufuku kubeba daftari na vitabu vya shule mkononi.

#### **6.0:VIFAA VYA KAZI/USAFI.**

Mwanafunzi aje na fagio kwa ajili ya usafi wa nje.

#### **8.0:SHERIA ZA SHULE**

Baadhi ya sheria za shule zimeambatanishwa na mwanao anaagizwa kuzisoma na kuzingatia ili asome bila shida.

#### **9.0:LUGHA YA KIINGEREZA.**

Wanafunzi wengi wanashindwa kupata Elimu ya Sekondari sawasawa na kushindwa katika mitihani kwa sababu hawajui Kiingereza.Mtoto wako atakapofika hapa shuleni lazima ajitahidi kujifunza lugha ya Kiingereza kwa guvu zote ili aweze kumudu masomo ya sekondari,bila kufanya hivyo mwanao atakuwa amekuja kupoteza muda bila mafanikio.Tafadhali msisitize mwanao juu ya suala hili muhimu.

#### **10:RIPOTI YA MAENDELEO YA MWANAFUNZI.**

Kila inapofungwa shule hakikisha mwanao anakupatia ripoti yake ya maendeleo shuleni ili na wewe upate nafasi ya kusaidia walimu kumshauri na kumlea kimaadili na kitaaluma.

#### **11:KUTOFIKA SHULENI**

Kama mwanao hatafika shuleni toa taarifa ya maandishi vinginevyo mwanao asipofika shuleni kwa muda mrefu atakuwa amejifukuzisha shule.

12:Mwisho kwa niaba ya Watumishi wote wa **SHULE YA SEKONDARI KIVESA** namkaribisha mwanao na kumtakia mafanikio katika safari yake ndefu ya maisha ya shule.Shule inatarajia mzazi/mlezi utakuwa karibu na shule kwa kushirikiana katika kumlea mwanao vyema

---

\_\_\_\_\_  
THERESIA NAZARI

MKUU WA SHULE

**KIVESA SECONDARY SCHOOL**

**MEDICAL CERTIFICATE FORM**

To be completed by medical officer in respect of Form I-V Entrants

**Pupil's full Name:**.....

Age:.....

Blood Count(Red and White)

Stool:.....

Urinalysis:.....

Syphilis test:.....

T.B test:.....

Ears:.....

Chest:.....

Spleen:.....

Abdomen:.....

**ADDITIONAL INFORMATION** (eg:Physical defects or  
Impairments,infections,chronic or family disease etc)

.....  
.....  
.....  
.....  
.....  
.....  
.....  
.....

I certify the above is fit/unfit for admission into Secondary school.

Designation:.....

Station:.....

Date:.....

**Official stamp:**.....